



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI
ZA MITAA



HALMASHAURI YA MANISPAA YA
TEMEKE

Unapojibu tafadhali taja:

Tarehe: February 11, 2022

Kumb. Na. TMC/LD/TP/AZM/01/9

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA KUKUSANYA TAARIFA ZA ANWANI ZA MAKAZI NA
POSTIKODI:**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke anawatangazia wananchi wote wanaoishi katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, nafasi za kazi ya muda kwa kazi ya kukusanya taarifa kwenye zoezi la anwani za makazi, katika kata na mitaa ya manispaa ya Temeke.

1. SIFA ZA MWOMBAJI:

- a) Awe ni Mtanzania mwanze umri kuanzia miaka 18 na ni Mkazi wa Temeke.
- b) Awe na simu ya Android yenye uwezo wa kukaa na chaji kwa siku moja na kuendelea.
- c) Awe na Elimu ya kidato cha nne au chuo kinachotambulika na Serikali.
- d) Awe na barua pepe (Email address) na nywila (Password) inayofanya kazi.
- e) Awe na uwezo wa kutafsiri ramani.

2. MAJUKUMU:

- 1) Kukusanya taarifa za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma.
- 2) Kutuma taarifa (Data) kwenye mfumo wa anwani za makazi.
- 3) Kukusanya taarifa za wamiliki wa nyumba, viwanja na maeneo ya huduma kwa kwa kutumia mfumo wa Anwani za makazi.
- 4) Muda wa kazi utaihsa kwa kuzingatia mkataba wa kazi.

3. MAOMBI YAAMBATISHWE NA:

- 1) Nakala ya Cheti cha kuzaliwa/Kitambulisho cha NIDA.
- 2) Nakala ya Cheti cha kidato cha Nne na Vinginevyo.
- 3) Picha (Passport size 2)
- 4) Barua ya Maombi ipitishwe na Mtendaji wa kata na Mtaa katika eneo unaloishi.

4. **Maombi yatumwe kwa:**

MKURUGENZI WA HALMASHAURI

MANISPAA YA TEMEKE

S.L.P. 46343

DAR ES SALAAM.

5. Mwisho wa kupokea maombi ni Tarehe 15/2/2022. Saa 9.30 Alasiri

Nawasilisha.


E. Huruma, Mabelya
MKURUGENZI WA MANISPAA
TEMEKE